# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)

## Kuongezwa kwa muda wa kuthibitisha udahili

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inawatangazia waombaji waliochaguliwa na vyuo zaidi ya kimoja katika awamu ya kwanza ya udahili kuwa imeongeza muda wa kuthibitisha hadi Jumatano tarehe 13 Septemba 2018 saa sita usiku.

Muda uomeongezwa ili kuruhusu waombaji walioshindwa kujithibitisha kwa sababu zifuatazo:

- Kuchelewa kupata ujumbe mfupi wa simu (SMS) wenye namba maalum ya siri;
- Kupoteza line ya simu hivyo kushindwa kupokea ujumbe mfupi; au
- Kufuta ujumbe mfupi wa simu (SMS) wenye namba maalum ya siri.

Aidha Tume inapenda kusisitiza kuwa masuala yote yahusuyo *Confirmation Codes* yaripotiwe moja kwa moja kwenye vyuo husika kwa utatuzi wa haraka.

Imetolewa
na
**Katibu Mtendaji**
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania**
**10/09/2018**